TANGAZO LA SERIKALI Na. 492 la tarehe 21/7/2023

SHERIA YA USHURU WA STEMPU,
(SURA YA 189)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA STEMPU YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii, itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Stempu ya mwaka, 2023.

Tafsiri

2. Katika Amri hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 189

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Ushuru wa Stempu;

"Barrick Tanzania Mining Companies" maana yake ni Bulyanhulu Gold Mine Limited, North Mara Gold Mine na Pangea Minerals Limited zote zikiwa ni kampuni tanzu za Twiga Minerals Corporation, ambazo chini ya Makubaliano zinamilikiwa kwa pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Barrick International Limited na kusimamiwa na Twiga Minerals Corporation;

Sura ya 123

"haki ya madini" maana yake ni leseni zinazorejewa katika kifungu cha 7 cha Sheria ya Madini;

"Makubaliano" maana yake ni Makubaliano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Barrick Tanzania Mining Companies yaliyoingiwa tarehe 24 Januari, 2020 ambapo Twiga Minerals Corporation iliundwa; na

"ushuru wa stempu" maana yake ni ushuru wa stempu unaotolewa kwa hati ambao ungeweza kutozwa chini ya kifungu cha 5(1) cha Sheria unaotokana na upangaji mpya wa hisa au umiliki wa hisa na uhamishaji wa haki za madini kutoka Barrick Tanzania Mining Companies kwenda kwa Twiga

Minerals Corporation kwa mujibu wa Ibara ya 3.3 ya Makubaliano.

Msamaha

3. Ushuru wa stempu unaotokana na hati yoyote inayohusisha upangaji mpya wa hisa au umiliki wa hisa na uhamishaji wa haki za madini kutoka Barrick Tanzania Mining Companies kwenda Twiga Minerals Corporation, umesamehewa.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo mara baada ya kukamilika kwa upangaji mpya na uhamishaji wa haki za madini zinazorejewa chini ya aya ya 3.

Dodoma,
14 Julai, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMA MADELU,
*Waziri wa Fedha,*